



Child Care Subsidy

Child Care Subsidy husaidia na gharama za huduma ya kutunza watoto iliyoidhinishwa. Ikiwa unastahiki, tutailipa moja kwa moja kwa mtoa huduma wa kutunza mtoto wako ili kupunguza ada unayolipa.

Ili kustahiki lazima ukidhi yote ifuatayo:

- kumlea mtoto wa umri wa miaka 13 au chini ambaye hayupo shule ya sekondari, isipokuwa msamaha unatumika
- kutumia huduma ya kutunza watoto iliyoidhinishwa
- kuwajibika kwa kulipa ada ya huduma ya kutunza watoto
- kukidhi mahitaji ya makazi na chanjo.

Ili kukidhi mahitaji ya makazi, wewe au mwenzi wako lazima uishi au aishi nchini Australia na una mmoja wa ifuatayo:

- uraia wa Australia
- viza ya kudumu ya makazi
- viza ya Special Category
- aina fulani ya viza ya muda, kwa mfano, viza ya Partner Provisional au ya Temporary Protection.

Unaweza pia kukidhi mahitaji ya makazi ikiwa yoyote ya chini inatumika:

- wewe au mwenzi wako ni mwanafunzi wa nje wa nchi, kufadhiliwa na Serikali ya Australia ili kusoma nchini Australia
- wewe uko katika shida ya kifedha au hali maalum inatumika.

Unaweza kusamehewa baadhi ya vigezo hivi katika hali maalum.

Kiasi cha Child Care Subsidy unachoweza kupata

Kiasi cha Child Care Subsidy unachoweza kupata hulingana na zote za hapa chini:

- mapato ya familia yako
- idadi ya watoto katika utunzaji wako
- kikomo cha juu cha kiwango cha saa kinachotegemea na aina ya huduma ya mtoto iliyoidhinishwa unayotumia na umri wa mtoto wako
- hali ya familia yako na masaa ya shughuli zinazotambuliwa ambayo wewe na mwenzi wako anafanya.

Mapato ya familia

Tutatumia mapato ya familia yako ili kuhesabu kiasi cha Child Care Subsidy unachoweza kuipata. Utahitaji kutoa kadirio la mapato kila mwaka wa kifedha ili tunaweza kuhesabu kiasi cha Child Care Subsidy kulipia huduma ya utunzaji wa mtoto wako.

Kiasi cha Child Care Subsidy unachoweza kuipata kinaweza kubadilika ikiwa mapato yako yanabadilika. Ili kuhakikisha unapata kiasi sahihi cha Child Care Subsidy unahitaji kuangalia na kusasisha kadirio la mapato yako.

Unaweza kusoma zaidi kuhusu hii kwenye servicessaustralia.gov.au/incomeccs

Kuzuia

Ili kusaidia kupunguza uwezekano wa malipo ya ziada, tutazuia 5% ya Child Care Subsidy yako kila wiki mbili. Unaweza kabadilika kiasi ambacho tunazuia.

Unaweza kusoma zaidi kuhusu hii kwenye servicessaustralia.gov.au/incomeccs

Kusawazisha

Mwishoni mwa mwaka wa kifedha tunasawazisha malipo yako. Tunafanya hivi kwa kulingana kadirio la mapato yako na mapato yako halisi. Hii itahakikisha kuwa umepata kiasi sahihi cha ruzuku.

Ikiwa kadirio la mapato yako ni chini kuliko mapato yako halisi unaweza kuwa na malipo ya ziada ambayo utahitaji kulipa. Tutatumia Child Care Subsidy ambayo tulizuia ili kupunguza kiasi unachopaswa kulipa.

Ikiwa kadirio la mapato yako ni juu zaidi kuliko mapato yako halisi na hukupata Child Care Subsidy ya kutosha, tutalipa kiasi chochote kinachodai kwako moja kwa moja kwako. Hii itajumuisha Child Care Subsidy tuliyozuia.

Kwa habari zaidi kuhusu Child Care Subsidy balancing katika Kiingereza na lugha zingine, nenda kwa servicessaustralia.gov.au/ccsbalancing

Idadi ya watoto wako katika huduma ya utunzaji

Ikiwa una zaidi ya mtoto mmoja wa umri wa miaka 5 au chini katika huduma ya kutunza watoto, unaweza kupata kiwango cha juu cha Child Care Subsidy kwa mtoto mmoja au zaidi ya watoto wako.

Ikiwa unastahili:

- mtoto wako mkubwa mwenye umri wa miaka 5 au chini atapata kiwango cha kawaida cha Child Care Subsidy kilichopimwa kwa mapato,
- watoto wowote wadogo wanaweza kupata kiwango cha juu sana cha Child Care Subsidy.

Kiasi cha juu sana unachoweza kupata kwa mtoto mwenye kiwango cha juu sana ni 95%. Watoto wowote wa umri wa miaka 6 na juu watendelea kupata asilimia ya kawaida yako ya Child Care Subsidy.

Kiwango cha juu zaidi cha Child Care Subsidy hakitumiki kwa vikao vya utunzaji vya In Home Care.

Unaweza kusoma zaidi juu ya hii kwenye servicessaustralia.gov.au/higherccs

Kikomo cha juu cha kiwango cha saa

Kiasi cha Child Care Subsidy unachoweza kupata kitalingana na aina ya huduma ya watoto iliyoidhinishwa unayotumia, na umri wa mtoto wako.

Asilimia yako ya Child Care Subsidy itatumika ama kwa ada ya saa unayotozwa na huduma yako ya utunzaji wa mtoto, au kikomo cha juu cha kiwango cha saa, yoyote ambayo iko chini.

Activity Test

Masaa ya huduma ya kutunza mtoto yenye ruzuku unayoweza kupata kila wiki mbili yanalingana na hali yako na masaa ya shughuli zilizotambulishwa unayofanya. Tunaita hii activity test.

Shughuli zinazotambulishwa zinaweza kujumuisha:

- kazi ya kulipwa - ikiwa ni pamoja na likizo, kama vile likizo ya uzazi
- masomo na mafunzo
- kazi isiyolipwa katika biashara ya familia
- kutafuta kazi
- kujitolea
- kujijiri mwenyewe
- shughuli nyingine kutegemea kesi.

Ikiwa una mwenzi, tutaangalia viwango vyenu vyote vya shughuli. Tutatumia kiwango cha chini cha kiwango cha shughuli yako au ya mwenzi ili kuhesabu masaa yako ya huduma ya kutunza watoto yenye ruzuku.

Ili kuhakikisha unapata kiasi sahihi cha Child Care Subsidy unahitaji kuangalia na kusasisha activity test yako ikiwa hali yako au ya mwenzi wako ikibadilika.

Kwa habari zaidi, nenda kwa servicesaustralia.gov.au/your-activity-level-affects-child-care-subsidy

Jinsi ya kudai Child Care Subsidy

Ili kufanya madai mtandaoni unahitaji akaunti ya myGov na akaunti mtandaoni ya Centrelink. Akaunti yako ya myGov lazima iunganishwe na Centrelink.

Ikiwa huna akaunti ya myGov, nenda kwenye my.gov.au ili kuanzisha akaunti.

Kwa msaada wa kuanzisha akaunti yako ya myGov, nenda kwa servicesaustralia.gov.au/mygovguides

Tumia akaunti yako mtandaoni wa Centrelink katika myGov ili kudai Child Care Subsidy, toa taarifa yako na hati zozote zinazosaidia dai lako.

Additional Child Care Subsidy

Additional Child Care Subsidy hutoa msaada wa ziada wa ada yao ya utunzaji wa watoto kwa familia kadhaa. Lazima ustahiki kwa Child Care Subsidy ili kustahiki kwa Additional Child Care Subsidy. Kuna aina tofauti ambazo unaweza kuomba:

- Additional Child Care Subsidy (Grandparent). Hii husaidia na gharama ya utunzaji wa mtoto ikiwa wewe ni bibi au babu au bibi mkubwa au babu mkubwa ambaye ana utunzaji wa msingi wa mjukuu wako au mjukuu wako mkubwa. Ili kustahiki, lazima upate malipo ya msaada wa mapato.
- Additional Child Care Subsidy (Temporary Financial Hardship). Hayo hutoa msaada wa muda mfupi na gharama ya huduma ya mtoto ikiwa uko katika shida ya kifeha ya muda kutokana na hali zilizo nje ya uwezo wako.
- Additional Child Care Subsidy (Transition to Work). Hii husaidia na gharama ya utunzaji wa mtoto ikiwa unabadilika kutoka kwa malipo ya msaada wa mapato kwa kushiriki katika shughuli za kazi, masomo au mafunzo.

Kuna pia Additional Child Care Subsidy (Child Wellbeing) ambayo unaweza kuuliza huduma ya utunzaji wa mtoto wako kuhusu hiyo. Hii husaidia familia na watoto walio katika mazingira magumu au wasiojiweza. Mtoa huduma wa kutunza mtoto wako atahitaji kutuma ombi kwa niaba yako.

Jinsi ya kuomba kwa Additional Child Care Subsidy

Ili kuomba hii mtandaoni utahitaji kuwa na akaunti ya myGov na akaunti mtandaoni ya Centrelink. Akaunti yako ya myGov lazima iunganishwe na Centrelink.

Tumia akaunti yako mtandaoni ya Centrelink kupitia myGov ili kutoa taarifa yako na nyaraka zozote zinazounga mkono.

Kadiria msaada wako wa ada ya utunzaji wa mtoto

Unaweza kutumia Child Care Subsidy Calculator ili kuona viwango vyako vya Child Care Subsidy vinaweza kuwa nini na kiasi gani unachoweza kulipa kwa huduma ya kutunza watoto. Enda kwa startingblocks.gov.au

Kwa habari zaidi

- Nenda kwa servicesaustralia.gov.au/childcaresubsidy kwa habari zaidi katika Kiingereza.
- Nenda kwa servicesaustralia.gov.au/yourlanguage ambapo unaweza kusoma, kusikiliza au kutazama habari katika lugha yako.
- Piga simu kwa **131 202** kuongea nasi katika lugha yako kuhusu malipo na huduma za Centrelink.
- Tembelea kituo cha huduma.

Kumbuka: simu kutoka simu yako ya nyumbani kwenda nambari za simu za '13' kutoka popote nchini Australia zinatozwa kwa kiwango kamili. Kiwango hicho kinaweza kutofautiana kutoka bei ya simu ya mtaa na kinaweza pia kutofautiana na watoa huduma wa simu. Simu kwa nambari za simu za '1800' kutoka simu yako ya nyumbani ni bila malipo. Simu kutoka simu za umma na za mkononi zinaweza kupimwa kwa muda wao na kutozwa kwa kiwango cha juu zaidi.

Kanusho

Taarifa iliyomo katika chapisho hili inakusudiwa kama mwongozo pekee wa malipo na huduma. Ni wajibu wako kuamua kama ungependa kuomba malipo na kufanya maombi kuhusiana na hali yako mahususi.



Child Care Subsidy

Child Care Subsidy helps with the cost of approved child care. If you are eligible, we will pay it directly to your child care provider to reduce the fees you pay.

To be eligible you must meet all of the following:

- care for a child 13 years of age or younger who is not in secondary school, unless an exemption applies
- use an approved child care service
- be responsible for paying the child care fees
- meet residency and immunisation requirements.

To meet the residency requirements, you or your partner must be living in Australia and have one of the following:

- Australian citizenship
- a permanent residence visa
- a Special Category visa
- a certain temporary visa type, for example, a Partner Provisional or Temporary Protection visa.

You may also meet the residency requirements if any of the below apply:

- you or your partner are an overseas student, sponsored by the Australian Government to study in Australia
- you are in hardship or special circumstances apply.

You may be exempt from some of these criteria in specific circumstances.

How much Child Care Subsidy you can get

The amount of Child Care Subsidy you can get depends on all of the below:

- your family's income
- the number of children in your care
- the hourly rate cap based on the type of approved child care you use and the age of your child
- your family's circumstances and the hours of recognised activities you and your partner do.

Family income

We will use your family income to work out the amount of Child Care Subsidy you can get. You will need to provide an income estimate each financial year so we can calculate how much Child Care Subsidy to pay your child care service.

The amount of Child Care Subsidy you can get may change if your income changes. To make sure you get the right amount of Child Care Subsidy you need to check and update your income estimate.

You can read more about this at servicessaustralia.gov.au/incomeccs

Withholding

To help reduce the chance of an overpayment, we will withhold 5% of your Child Care Subsidy each fortnight. You can change the amount we withhold.

You can read more about this at servicessaustralia.gov.au/incomeccs

Balancing

At the end of the financial year we balance your payments. We do this by comparing your income estimate to your actual income. This will make sure you got the correct amount of subsidy.

If your income estimate is lower than your actual income you may have an overpayment which you will need to pay back. We will use the Child Care Subsidy we withheld to reduce the amount you have to pay back.

If your income estimate is higher than your actual income and you did not get enough Child Care Subsidy, we will pay any outstanding amount directly to you. This will include the Child Care Subsidy we withheld.

For more information about Child Care Subsidy balancing in English and other languages, go to [servicessaustralia/ccsbalancing](https://servicessaustralia.gov.au/ccsbalancing)

Number of children in care

If you have more than one child aged 5 or under in care, you may get a higher rate of Child Care Subsidy for one or more of your children.

If you are eligible:

- your eldest child aged 5 or under will get your standard income tested Child Care Subsidy rate,
- any younger children may get a higher rate of Child Care Subsidy.

The most you can get for your higher rate child is 95%. Any children aged 6 and above will continue to get your standard Child Care Subsidy percentage.

The higher Child Care Subsidy rate does not apply to In Home Care sessions of care.

You can read more about this at servicessaustralia.gov.au/higherccs

Hourly rate cap

The amount of Child Care Subsidy you can get will depend on the type of approved child care you use and the age of your child.

Your Child Care Subsidy percentage will apply to either the hourly fee you are charged by your child care service or the hourly rate cap, whichever is lower.

Activity Test

The hours of subsidised child care you can get each fortnight depends on your circumstances and the hours of recognised activities you do. We call this an activity test.

Recognised activities can include:

- paid work – including leave, like maternity leave
- study and training
- unpaid work in family business

- looking for work
- volunteering
- self-employment
- other activities on a case-by-case basis.

If you have a partner, we will look at both of your activity levels. We will use the lower of your or your partner's activity level to work out your hours of subsidised child care.

To make sure you get the right amount of Child Care Subsidy you need to check and update your activity test if your or your partner's circumstances change.

For more information, go to servicessaustralia.gov.au/your-activity-level-affects-child-care-subsidy

How to claim Child Care Subsidy

To make a claim online you need a myGov account and a Centrelink online account. Your myGov account must be linked to Centrelink.

If you do not have a myGov account, go to my.gov.au to create one.

For help setting up your myGov account, go to servicessaustralia.gov.au/mygovguides

Use your Centrelink online account in myGov to claim Child Care Subsidy, provide your information and any supporting documents.

Additional Child Care Subsidy

Additional Child Care Subsidy offers some families extra help with their child care fees. You must be eligible for Child Care Subsidy to be eligible for Additional Child Care Subsidy. There are different types you can apply for:

- Additional Child Care Subsidy (Grandparent). This helps with the cost of child care if you are a grandparent or great grandparent with primary care of your grandchild or great grandchild. To be eligible, you must get an income support payment.
- Additional Child Care Subsidy (Temporary Financial Hardship). This gives short-term help with the cost of child care if you are in temporary financial hardship due to circumstances beyond your control.
- Additional Child Care Subsidy (Transition to Work). This helps with the cost of child care if you are transitioning from an income support payment by engaging in work, study or training activities.

There is also Additional Child Care Subsidy (Child Wellbeing) which you can ask your child care service about. This helps vulnerable or disadvantaged families and children. Your child care provider will need to apply on your behalf.

How to apply for Additional Child Care Subsidy

To apply online you need a myGov account and a Centrelink online account. Your myGov account must be linked to Centrelink.

Use your Centrelink online account through myGov to provide your information and any supporting documents.

Estimate your child care fee assistance

You can use the Child Care Subsidy Calculator to see what your Child Care Subsidy rates may be and how much you may pay for child care. Go to startingblocks.gov.au

For more information

- Go to servicesaustralia.gov.au/childcaresubsidy for more information in English.
- Go to servicesaustralia.gov.au/yourlanguage where you can read, listen to or watch information in your language.
- Call **131 202** to speak with us in your language about Centrelink payments and services.
- Visit a service centre.

Note: calls from your home phone to '13' numbers from anywhere in Australia are charged at a fixed rate. That rate may vary from the price of a local call and may also vary between telephone service providers. Calls to '1800' numbers from your home phone are free. Calls from public and mobile phones may be timed and charged at a higher rate.

Disclaimer

The information contained in this publication is intended only as a guide to payments and services. It's your responsibility to decide if you wish to apply for a payment and to make an application with regard to your particular circumstances.